

Namna ya Kufanya Maombi ya 3SquaresVT Mpango wa Vermont wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada (Supplemental Nutrition Assistance Program)

(Ilikuwa ikiitwa Food Stamps)

1. Jaza na utume fomu yako ya maombi kwa Economic Services Division ya karibu yako.

Ili upate fomu za maombi, tazama **www.vermontfoodhelp.com** au piga simu **1-800-287-0589**. Kwa usaidizi wa kujaza fomu ya maombi, piga simu **Community Action Agency** ya eneo lako (kama hujui namba yao, piga simu **2-1-1**). Wazee wanaweza kupiga simu Usaidizi kwa Wazee (Senior Helpline) kwa **1-800-642-5119**.

2. Mahojiano na mhudumu wako wa 3SquaresVT.

Baada ya kupokea maombi yako, Huduma za Kiuchumi (Economic Services) watakutumia barua itakayokuwa na tarehe na wakati wa mahojiano yako. Watu wengi wanaweza kuwa na mahojiano kupitia simu. Muulize muhudumu wako wa 3SquaresVT.

3. Unayotakiwa kutayarisha kwa mahojiano yako ya 3SquaresVT:

Mahitaji:

- ♦ Thibitisho la kitambulisho [Namba ya Hazina ya Jami (Social Security Number - na kitambulisho cha binafsi)]
- ♦ Thibitisho la mapato yote (kwa mfano: nakala za malipo, nakala za benki, nk.)

Ya Ziada – ili uweze kupata marupurupu mengi zaidi:

- ♦ Gharama za nyumbani na za matumizi (kwa mfano: risiti ya kodi, nakala ya malipo ya mkopo wa nyumba, bili za simu, nk.)
- ♦ Gharama za matibabu kama una umri wa zaidi ya miaka 60 au una ulemavu (kwa mfano: billi, malipo, viwango vya malipo, nk.)
- ♦ Huduma kwa watoto au wazee (kwa mfano: hundi iliyolipwa au hati kutoka kwa mpeana huduma)
- ♦ Malipo ya usaidizi wa watoto ulioamrisha na mahakama (thibitisho la malipo)



**Vermont Campaign to
End Childhood Hunger**

*This message is funded in part by the USDA,
an equal opportunity provider and employer.*

4/10/09

 **VERMONT**
DEPARTMENT FOR CHILDREN AND FAMILIES
ECONOMIC SERVICES DIVISION

Inakuwaje baada ya kufanya maombi?

Inaweza kuchukua hadi siku 30 kwa Idara ya Huduma za Kiuchumi [Economic Services Division (ESD)] kukamilisha maombi yako. Kama hujapata mawasiliano kutoka kwa ESD baada ya siku 20, piga simu kwa ofisi yako ya wilaya ufwatilie hali ya maombi yako.

Ukiidhinishwa kupata marupurupu ya 3SquaresVT, utapokea barua ya tuzo kupitia posta itakayokueleza kiwango cha marupurupu yako ya kila mwezi.

Nyumba ambazo kila mtu ni mzee (miaka 65 au zaidi) au anapokea Mapato ya Ziada ya Jamii [SSI (Supplemental Security Income)], kila mwezi, marupurupu yao yatawekwa moja kwa moja katika akaunti zao za benki.

Nyumba nyengine zote zitapokea kadi ya EBT (Hawala ya Marupurupu Kupitia Umeme) kupitia posta.

Mara tu ukishachagua namba yako ya pin, utakuwa tayari kutumia kadi yako. Inakubalika katika maduka mengi ya vyakula na pia katika masoko kadhaa ya wakulima Vermont na inatumika kama kadi ya mtoe (debit) au ya mkopo (credit).

Marupurupu yatawekwa kwenye kadi yako mwanzo wa kila mwezi.

Huduma za Kiuchumi watawasiliana nawe wakati ukifika kukagua kesi yako, ambayo ni kwa muda wa miezi 12 hadi 24 kwa nyumba nyingi.

Ukinyimwa marupurupu, una haki ya kukata rufani. Wapigie simu Legal Aid ndio upate usaidizi: 1-800-769-7459.

